JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HADIDU ZA REJEA

# TUME YA RAIS YA KUFANYA TATHMINI YA MASUALA YA ARDHI KATIKA UTEKELEZAJI WA UAMUZI WA SERIKALI KUHUSU UHAMAJI WA HIARI WA WAKAZI WA ENEO LA HIFADHI LA NGORONGORO

DODOMA JANUARI, 2025

## 1.0 UTANGULIZI

Mfumo wa umiliki na matumizi mseto ya ardhi katika eneo la Hifadhi la Ngorongoro umekuwepo tangu kuanzishwa kwa eneo hilo mwaka 1959, kwa lengo la kutimiza majukumu matatu ya uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii kwa uwiano. Hata hivyo, usimamizi wa eneo hilo umeshindwa kutimiza lengo la kuleta uwiano huo kutokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo na mifugo ikilinganishwa na ukubwa wa ardhi iliyopo na hivyo, kuathiri masuala ya ustawi wa jamii, uhifadhi na ikolojia ya eneo hilo.

Kufuatia hali hiyo, Serikali kwa nyakati tofauti imechukua hatua mbalimbali katika kupata ufumbuzi wa changamoto za usimamizi wa Hifadhi kwa kuzingatia matokeo ya tafiti zilizofanyika, na mapendekezo ya kamati mbalimbali zilizoundwa, hatua ambayo haikuleta utatuzi wa kudumu wa changamoto hizo. Kutokana na umuhimu wa suala hili, Serikali iliamua kutoa fidia na motisha kwa wenyeji wa eneo la Hifadhi la Ngorongoro waliokuwa tayari kuhamia Msomera na maeneo mengine kwa hiari.

Hata hivyo, yamejitokeza malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na wadau mbalimbali kuhusu madai ya ukiukwaji wa taratibu na kutoshirikishwa ipasavyo. Aidha, mnamo tarehe 01 Disemba, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya mkutano na viongozi wa kimila wa jamii ya Kimasai (Malaigwanani) wanaoishi katika eneo la Ngorongoro. Baada ya kusikiliza hoja na malalamiko yao, Mheshimiwa Rais aliahidi kuunda Tume kwa lengo la kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya ardhi na utekelezaji wa zoezi la uhamaji wa hiari.

## 2.0 LENGO MAHSUSI

Kufanya tathmini na uchambuzi wa kina kuhusu masuala ya ardhi iliyopo katika Hifadhi ya Ngorongoro ikiwa ni pamoja na kuangalia mfumo wa umiliki, matumizi ya ardhi na changamoto zilizopo ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki zitakazoboresha na kuimarisha mazingira ya eneo hilo ambalo ni muhimu kwa ajili

ya utunzaji mazingira, bioanuai na utalii pamoja na kuendelea kulinda hadhi ya Hifadhi kitaifa, kikanda na kimataifa.

## 3.0 HADIDU ZA REJEA

Ili kutekeleza kazi hiyo, Tume itaongozwa na Hadidu za Rejea zifuatazo :-

3.1 Kufanya uchambuzi wa nyaraka kuhusu historia ya Hifadhi ya Ngorongoro, hadhi yake, umuhimu wake uendelezaji na matumizi mseto ya ardhi ndani ya Hifadhi.

3.2 Kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu Hifadhi ya Ngorongoro yakiwemo:

a) Lengo la uhifadhi;
b) Kubaini migogoro iliyopo na vyanzo vyake;
c) Kufanya tathmini ya athari za migogoro kijamii, kiuchumi, kimazingira, kisiasa na kimataifa; na
d) Kufanya tathmini ya ushirikishwaji wa wananchi katika upangaji na umilikishaji wa ardhi ndani ya eneo la Ngorongoro.
e) Kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa zote muhimu zitakazopatikana kuhusu Maisha na Uhifadhi ndani ya Wilaya ya Ngorongoro.

3.3 Kufanya uchambuzi wa mfumo wa ukaaji na utumiaji wa ardhi ndani ya Hifadhi kwa mazingira ya sasa.

3.4 Kufanya tathmini ya athari na uendelevu wa matumizi mseto ya ardhi katika eneo la Hifadhi la Ngorongoro;

3.5 Kuangalia hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika vipindi tofauti katika kushughulikia masuala ya uhifadhi na maisha ya wakazi wa eneo la Hifadhi la Ngorongoro;

3.6 Kufanya tathmini ya athari za ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa ustawi wa maisha ya wananchi na mabadiliko ya tabia nchi katika eneo la Hifadhi la Ngorongoro na hatua zinazochukuliwa na Serikali;

3.7 Kufanya tathmini ya mitizamo ya wadau kuhusu Hifadhi ya Ngorongoro;

3.8 Kufanya tathmini ya mwitikio wa jamii ya Maasai kuhusu jitihada mbalimbali zilizofanywa na Serikali kuhusu Maisha na Uhifadhi katika Wilaya ya Ngorongoro;

3.9 Kubaini na kushauri namna bora ya kuwaandaa wananchi wanaohama kutoka kutegemea ufugaji pekee na kuwa na mfumo mbadala wa kuendesha maisha yao;

3.10 Kufanya uchambuzi wa faida na hasara za kijamii na kiuchumi ambazo wananchi wanazipata kwa kukaa na kuishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro;

3.11 Kufanya tathmini ya hali halisi ya maisha na upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi wanaoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikilinganishwa na maeneo mengine yanayofanana na Ngorongoro; na

3.12 Kushauri masuala mengine ambayo Tume itaona kuwa ni muhimu kuzingatiwa katika kupata suluhu ya kudumu ya migogoro ya ardhi katika eneo la Hifadhi.

## 4.0 MATOKEO TARAJIWA

Kuandaliwa kwa taarifa ya kina inayobainisha matokeo ya tathmini na mapendekezo ya hatua za kuchukua kwa lengo la kuboresha namna ya utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhusu uhamaji wa hiari kutoka eneo la Hifadhi la Ngorongoro.

## 5.0 MUDA WA KAZI

Tume inatarajiwa kukamilisha kazi yake ndani ya kipindi cha miezi mitatu (3) kuanzia tarehe ya uzinduzi.

## 6.0 UWAJIBIKAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA YA TUME

Tume itawajibika na kuwasilisha Taarifa yake kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, Tume itawasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi taarifa yake ya awali (*inception report*) ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuanza kazi, rasimu ya kwanza ndani ya siku arobaini na tano (45) na taarifa kamili baada ya kukamilisha kazi.